#WeweNdoFuture
#TimizaWajibu

HESLB Yako

Jarida la Mtandaoni la Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu | Toleo Na. 2

Aprili - Juni 2021

# TZS 570bn KWA WANAFUNZI 160,000



**Na Mwandishi Wetu**
**Dar es salaam**

SERIKALI kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imepanga kutumia bajeti ya kiasi cha TZS 570 Bilioni katika mwaka 2021/2022 inayotarajia kuwanufaisha zaidi ya wanafunzi 160,000.

Akizungumza (Ijumaa, Julai 2, 2021) jijini Dar es salaam katika hafla ya uzinduzi wa msimu mpya wa uombaji mikopo kwa mwaka wa masomo 2021/2022, Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako amesema kiwango cha fedha kilichotengwa kwa 2021/2022 kimevunja rekodi katika miaka 16 ya uhai wa HESLB.

Kwa mujibu wa Prof. Ndalichako, kati ya wanafunzi hao 160,000, wanafunzi wa mwaka wa kwanza wanatarajiwa kuwa 62,000 wakati wanaoendelea na masomo watakua 98,000.

"Niwaibie siri tu. Hadi mwezi uliopita, bajeti ya mikopo kwa mwaka 2021/2022 ilikua TZS 500 bilioni. Lakini katika siku zake 100 za uongozi kama Rais wetu, Mhe. Mama Samia Suluhu Hassan ameongeza TZS. 70 bilioni na kufikia hizi TZS. 570 bilioni kwa mwaka 2021/2022 sawa sawa na ongezeko la TZS. 106 bilioni (22.8%)" alisema Prof. Ndalichako.

Aliongeza kuwa ongezeko hilo linathibitisha nia ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mama Samia Suluhu Hassan ni kuendelea kuwawezesha vijana wengi kupata fedha na kusoma ili watumikie nchi yao na kuwataka waombaji wahitaji watulie, na kusoma maelekezo na kuomba kwa usahihi ili watimize ndoto zao.

Katika mwaka wa masomo wa 2020/2021, Serikali imetenga na kutoa TZS 464 bilioni zinazowanufaisha jumla ya wanafunzi 149,398. Kati yao, wanafunzi 55,287 ni wa mwaka wa kwanza na wengine 94,111 ni wale wanaoendelea na masomo.

Aidha katika hatua nyingine, Prof. Ndalichako aliitaka HESLB kuendelea kutoa elimu ya kutosha kwa waombaji ili waweze kuelewa sifa na utaratibu wa kuomba mkopo kwa usahihi na kuendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuwasaidia vijana wengi wanaoomba mikopo.

Akizungumza katika hafla hiyo iliyofanyika katika ofisi za HESLB, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru amesema wamepokea maelekezo na kuanzia Julai 12 mwaka huu, maafisa wa HESLB wataanza kuendesha programu za elimu ya uombaji mikopo kwa usahihi chini ya kampeni ya #WeweNdoFuture.

"Tunakamilisha utaratibu na uongozi wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ili tuwafikie vijana wote waliopo katika kambi 19 za JKT kuanzia Julai 12 … tutaendesha pia programu hizi kupitia televisheni, redio, mitandao ya kijamii na mikutano na wadau," amesema Badru.

Kuhusu utaratibu na muda wa kuomba, Badru amesema Mwongozo wa Uombaji mkopo unaoeleza sifa na utaratibu wa kuomba mkopo unapatikana katika www.heslb.go.tz kuanzia leo (Ijumaa, Julai 2, 2021).

"Mwongozo upo katika tovuti kuanzia leo, Julai 2 na tunawashauri waombaji wausome kabla ya kuomba. Aidha, mfumo wa kupokea maombi kuwa wazi kwa siku 53 kuanzia, Julai 9 hadi Agosti 31, 2021," amesema Badru.

Mkutano huo wa uzinduzi pia uliohudhuriwa na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe na wawakilishi kutoka Shirika la Posta Tanzania (TPC) na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) ambao pia huwahudumia waombaji mikopo.

HESLB ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria, ikiwa na majukumu makuu ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wahitaji na kukusanya mikopo iliyoiva iliyotolewa na Serikali kwa wanafunzi wa elimu ya juu tangu mwaka 1994/1995.



**Ismail Ngayonga**
*Mhariri*

## TUMEJIPANGA, TUPO TAYARI KWA KAZI

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hivi karibuni lilijadiliwa na kupitisha Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2021/2022 ya kiasi cha TZS 1.3 Trilioni.

Kati ya fedha hizo, kiasi cha TZS 570 Bilioni kilitengwa kwa ajili ya kugharamia mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, ambalo ni ongezeko la kiasi cha TZS 16 Bilioni ikilinganishwa na bajeti ya TZS 464 iliyotolewa na Serikali katika mwaka wa fedha 2020/2021.

Ongezeko hilo la bajeti ni dhamira ya dhati ya Serikali ya kuhakikisha kuwa HESLB inaendelea kutoa mikopo wa wanafunzi wahitaji ili kuweZa kuzalisha vijana wengi zaidi wenye ujuzi maarifa na taaluma mbalimbali ili kuliletea maendeleo ya taifa letu.

Aidha, kuongezeka kwa bajeti ya mkopo ni moja ya mikakati ya HESLB inayolenga katika kuimarisha usimamizi wa hali ya utulivu, umoja na mshikamano wa taasisi za elimu ya juu nchini na kuendeleza hali ya ustawi bora wa maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Ni ukweli ulio wazi kuwa katika kipindi cha miaka sita sasa, stahiki na malipo yote ya fedha zote za wanafunzi na vyuo zimekuwa zikilipwa kwa wakati. Hii ni udhibitisho kuwa Serikali kupitia HESLB imeendelea kutoa ushirikiano mkubwa kwa menejimenti za vyuo, na serikali za Jumuiya za wanafunzi vyuoni.

HESLB inawahakikisha wanafunzi na wadau wote kuwa itaongeza kasi katika utoaji na upangaji mikopo kwa mwaka 2021/2022. Tunaziomba mamlaka zinazohusika kuendeleza mashirikiano yaliyopo ili kujenga taasisi na jumuiya imara za sekta ya elimu ya juu nchini..

HESLB tumejipanga na tupo tayari kwa kazi, tunawatakia heri wadau wetu wote katika kufunga mwaka wa masomo 2020/2021 na kuwakaribisha katika mwaka mpya wa masomo 2021/2022.


## NDANI...



07 KITIKU: UDOSO TUTAENDELEA KUUNGA MKONO SERIKALI



08 MHE. HEMEDI TAHLISO; KAZI NZURI



11 UONGOZI MPYA TAHLISO WAIPONGEZA SERIKALI



12 JUSTA: HESLB MLEZI WA WANA

BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Abdul-Razaq Badru

**Katibu**
Omega Ngole

**Wajumbe**
Veneranda Malima
Ismail Ngayonga
Eline Maronga
Jonathan Nkwabi
Jacqueline Msuya

**Designer**
+255 719 190 083

**Mawasiliano**
Mkurugenzi Mtendaji
Bodi ya Mikopo ya
Wanafunzi wa Elimu ya Juu
1 Mtaa wa Kilimo, TAZARA
S.L.P 76068
Dar es salaam
Tanzania

**WhatsApp:** 0736 665 533
**Barua Pepe:** adcp@heslb.go.tz
**Tovuti:** heslb.go.tz

HESLB
BODI YA MIKOPO
INVESTING IN THE FUTURE

# MEZA YA MWENYEKITI



**Aidha kabla ya kufunguliwa kwa dirisha la maombi, HESLB inatarajia kutangaza mwongozo wa uombaji mikopo kwa mwaka 2021/2022 unaoainisha sifa, vigezo na taratibu za uombaji mikopo kwa wanafunzi wahitaji.**

**Na Mwandishi Wetu**
**Dar es salaam**

Karibuni Wasomaji wetu katika toleo Na. 2 la Jarida la mtandaoni la HESLB Yako, ambalo kimsingi ni taswira na kiungo cha mawasiliano kati ya HESLB na wadau wetu.

Julai 9 mwaka huu, HESLB inatarajia kufungua dirisha la maombi ya mkopo wa elimu ya juu kwa njia ya mtandao, na kutoa fursa kwa wanafunzi wahitaji kuwasilisha maombi yao kwa ajili ya upangaji wa mikopo.

Aidha kabla ya kufunguliwa kwa dirisha la maombi, HESLB inatarajia kutangaza mwongozo wa uombaji mikopo kwa mwaka 2021/2022 unaoainisha sifa, vigezo na taratibu za uombaji mikopo kwa wanafunzi wahitaji.

Tunachukua fursa hii kuwakumbusha wadau wetu wakiwemo wanafunzi, wazazi na walezi, kuanza maandalizi ya uombaji mikopo kwa kuandaa nyaraka muhimu zinazohitajika kama zitavyokavyoainishwa kupitia mwongozo utakaotolewa.

Ni wajibu wa wanafunzi wahitaji, wazazi na walezi kusoma mwongozo huo kwa umakini na kuelewa mahitaji ya msingi na hivyo kuepuka makosa yanayoweza kujitokeza pindi wanapofanya maombi hayo kupitia njia ya mtandao.

Aidha katika jitihada za kusaidia wanafunzi wahitaji, HESLB kwa kushirikiana na wadau mbalimbali hivi karibuni itaanza ziara ya kutembelea mikoa mbalimbali nchini ili kutoa elimu kwa waombaji kupitia vyombo vya habari, kambi za Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na mikutano ya ana kwa ana kwa kutoa ufafanuzi wa hoja zitakazojitokeza.

Ili kuongeza kasi ya ufanisi na utendaji wa mifumo yetu ya kitaasisi katika msimu ujao wa masomo 2021/2022 HESLB tayari imesaini hati ya makubaliano (MoU) na Wakala wa Usajili, Ufulisi na Udhamini (RITA) pamoja na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar (ZHELB), ambao kimsingi ni wadau muhimu katika mchakato wa maombi ya mkopo.

Tunawahakikishia wadau wetu kuwa katika mwaka wa masomo 2021/2022, HESLB imejipanga kuongeza kasi, nguvu na ari katika kuendelea kulipa fedha na stahili za wanafunzi kwa wakati na kushughulikia changamoto mbalimbali pindi zinapojitokeza.

Kupitia jarida hili ambalo linatoa tafsiri ya majukumu ya kisheria ya HESLB, tutaendelea kupokea maoni, hoja na ushauri ili kuboresha zaidi huduma zetu kwa maslahi mapana ya wadau wetu.

**Karibuni sana!**

# EMMANUEL MARTINE:

## TUJENGE MAHUSIANO MAZURI NA MENEJIMENTI ZA VYUO



**Na Ismail Ngayonga**
**Dodoma**

Jumuiya ya Serikali za Wanafunzi wa taasisi za elimu ya juu nchini wametakiwa kuimarisha ushirikiano na menejimenti za vyuo ili kutoa taarifa sahihi zenye kuzingatia maslahi mapana ya wanafunzi na taifa kwa ujumla.

Rai hiyo imetolewa na Naibu Kamishna wa Mikopo, Mipango na Fedha wa TAHLISO, Emmanuel Martine wakati wa mahojiano yake na HESLB Yako kuhusiana na ushindi alioupata hivi karibuni wa TUZO ya Kiongozi Bora wa Serikali ya Wanafunzi katika Chuo Kikuu Dodoma (UDOM).

Emmanuel Martine, ambaye ni Mwanafunzi wa mwaka wa tatu katika Chuo Kikuu Dodoma, anabainisha siri ya utatu (menejimenti za vyuo, serikali za wanafunzi na taasisi za serikali kuwa ni nguzo muhimu katika kushughulikia hoja na changamoto za wanafunzi.

Emmanuel alisema kiongozi wa serikali ya wanafunzi anapaswa kujenga mahusiano ya karibu na menejimenti ya chuo katika kuwasilisha hoja na changamoto za wanafunzi na kutoa taarifa sahihi na kwa wakati ili kuepuka migongano isiyo na maslahi.

"Suala la mikopo ya wanafunzi ni jambo lionalobeba maslahi ya wengi, ni wajibu wa menejimenti na serikali za wanafunzi kushirikiana pamoja katika utoaji wa taarifa sahihi ili kukuza ustawi wa taasisi za elimu ya juu" alisema Martine.

Aidha, Martine aliishukuru Menejimenti ya HESLB kwa ushirikiano mkubwa inaoutoa kwa serikali za wanafunzi wa taasisi za elimu ya juu kwani umekuwa msaada mkubwa katika kusaidia hali ya umoja na mshikamano wa wanafunzi vyuoni.

Akizungumzia kuhusu ushindi wa tuzo ya Kiongozi bora, Emmanuel alisema tuzo hiyo imetolewa kufuatia ushindi wa kura 23,000 alioupata kutoka kwa wadau mbalimbali ikiwemo Menejimenti ya UDOM, taasisi za kifedha na wanafunzi wa UDOM kutokana na mchango aliounyesha katika nafasi yake ya Waziri wa Mikopo katika jumuiya ya UDOSO.

"Niliingia madarakani mwaka 2019, nikiwa waziri wa mikopo nilijituma sana katika kuwasaidia wanafunzi wenzangu, nilijenga mahusiano mazuri na Menejimenti katika kushughulikia hoja na changamoto zetu. Naishukuru HESLB ilinipa msaada mkubwa hadi leo hii", alisema Emmanuel.

Kwa mujibu wa Emmanuel anasema ni wajibu wa viongozi wa serikali za wanafunzi kuwa na mlengo chanya wakati wa kuwasilisha hoja na changamoto za wanafunzi kwa menejimenti za vyuo, kwani viongozi hao wamebeba taswira na maslahi mapana ya wanafunzi.

**"Suala la mikopo ya wanafunzi ni jambo lionalobeba maslahi ya wengi, ni wajibu wa menejimenti na serikali za wanafunzi kushirikiana pamoja utoaji wa taarifa sahihi ili kukuza ustawi wa taasisi za elimu ya juu" alisema Emmanuel**




**Juni 7, 2021:** Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru (kushoto) akionesha kwa waandishi wa vyombo vya habari Hati ya Makubaliano (MoU) kati ya HESLB na Wakala wa Usajili, Udhamini na Ufilisi (RITA).



**Aprili 29, 2021:** Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru akisaini Hati ya Makubaliano (MoU) na Mkurugenzi wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar (ZHELB) Idd Khamis Haji katika Hafla iliyofanyika Zanzibar.



**Mei 25, 2021:** Mwenyekiti mstaafu wa TAHLISO Peter Niboye akimkabidhi taarifa ya utekelezaji wa Jumuiya hiyo, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) Hemed Suleiman Abdulla wakati wa mkutano baina yao uliofanyika Zanzibar.



**Aprili 16, 2021:** Mkurugenzi wa Fedha na Utawala HESLB, Neema Kuwite akimkabidhi cheti cha ushiriki wa mafunzo ya kuhudumia wateja, Afisa Mikopo Mkuu, Rose Malo.



**Mei 31, 2021:** Afisa Mawasiliano Mwandamizi HESLB, Ismail Ngayonga akitoa ufafanuzi kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Chinangali Jijini Dodoma wakati walipotembelea banda la HESLB katika maonesho ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufunzi (NACTE).



Mkurugenzi Msaidizi wa Urejeshaji Mikopo (HESLB), Deus Changala akipeana mkono na mmoja wa waajiri bora waliopatiwa tuzo na HESLB wakati wa Maonesho ya Mikopo Day yaliyofanyika tarehe 27-28 Mei Jijini Mbeya.

# TUZO KWA WAREJESHAJI (WAAJIRI) 10 BORA

**Na Jacqueline Msuya, Mbeya**
**Mbeya**

**“Nawapongeza waajiri wote kwa ushirikiano mzuri mliouonesha kwa HESLB. Nawasihi waajiri wengine waendelee kujiitokeza na kuanza kuwasilisha makato yao HESLB ili kuwa na mfuko endelevu”, alisema Changala.**

HESLB imetoa tuzo ya utambuzi kwa waajiri kumi bora wanaozingatia sheria ya urejeshaji wa mikopo ya elimu ya juu kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Jijini Mbeya.

Akizungumza wakati wa hafla ya utoaji wa tuzo hizo, iliyofanyika hivi karibuni Jijini Mbeya, Mkurugenzi Msaidizi wa Urejeshaji Mikopo (HESLB), Deus Changala alisema malengo ya tuzo hizo ni kujenga hamasa ya urejeshaji wa mikopo ya elimu kwa waajiri na wanufaika.

"Nawapongeza waajiri wote kwa ushirikiano mzuri mliouonesha kwa HESLB. Nawasihi waajiri wengine waendelee kujiitokeza na kuanza kuwasilisha makato yao HESLB ili kuwa na mfuko endelevu", alisema Changala.

Aliongeza kuwa waajiri hao wanasimamia marejesho ya 15% ya makato ya mshahara, na kwamba mwaka huu HESLB imewaenzi wakuu wa Taasisi hizo kumi zinazofanya vizuri zaidi katika marejesho katika Mkoa wa Mbeya.

Kwa mujibu wa Changala, tangu miaka ya nyuma HESLB imekuwa ikitoa tuzo mbalimbali za utambuzi kwa wadau. Mwaka 2021, HESLB imekuja na tuzo muhimu kwa lengo la kutoa motisha kwa waajiri wengine kuwasilisha marejesho kwa wakati.

Akizungumza na HESLB Yako, Mkuu wa Chuo cha Catholic University of Mbeya (CUCOM) Prof. Romuald Haule ambayo ni mmoja wa washindi wa tuzo hizo alisema, Menejimenti ya CUCOM inaipongeza HESLB kwa kuitunuku tuzo hiyo ambayo kimsingi imedhihirisha juhudi zao katika matakwa ya Sheria ya urejeshaji wa mikopo.

"Uongozi na jumuiya nzima ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Kikatoliki Mbeya (CUCoM) tunapenda kutumia fursa hii kuishukuru Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Tanzania (HESLB), hii ni heshima kubwa kwetu, tumefarijika na tunaahidi kuwa tutaendelea kuipalilia jadi hii adhimu" alisema Prof. Haule.

Waajiri kumi waliopatiwa tuzo ni pamoja na taasisi ya Wildlife Conversation Society, Wakulima Tea Co. Ltd, Coca Cola Kwanza Ltd, SBC Tanzania Ltd,HJF Medical Research International, Pandahill Secondary, St. John College of Health Science, Catholic University College of Mbeya, Uyole Health science Institute na Lafarge Tanzania Limited





# YOCTAN; HAKUNA 'KUBEBWA' MIKOPO ELIMU YA JUU

**Na Jacqueline Msuya, Morogoro**

Yoctan Mwamwingi (27) anataja siri ya kupangiwa mkopo wa elimu ya juu kwa asilimia 100 ilitokana na kuzingatia maelekezo yaliyotolewa katika mafunzo ya uombaji mikopo yaliyoendeshwa na HESLB Jijini Mbeya, mwezi Julai mwaka 2020.

Yoctan ni mwanafunzi katika Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA) Mkoani Morogoro, mtoto pekee katika familia ya Mzee Lucas Mwamwingi (54) na Bi. Lupoke Mwambeta (46) ambao ni wakulima, wakazi Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

"Naishukuru HESLB, kunipanga mkopo kwa 100%. Mafunzo ya mwaka 2020 yalinisaidia sana. Kwa hali ya kiuchumi ya familia yangu ingekuwa ngumu kumudu gharama za elimu kuanzia ada ya masomo na kadhalika" alisema Yoctan.

Yoctan anasema katika mafunzo hayo yaliyoendeshwa na Maafisa wa HESLB, yalihudhuriwa na wanafunzi 2000 kutoka Shule za Sekondari na vyuo vya kati katika Jiji la Mbeya, yaliwasaidia kupata uelewa wa pamoja kuhusu taratibu za uombaji mikopo ya elimu ya juu.

Anaongeza kuwa HESLB imekuwa mkombozi kwa wanafunzi wahitaji kutoka katika kaya maskini, kwani kwa sasa wazazi wengi katika familia hizo wameondokana na msongo wa mawazo katika kusomesha vijana wao masomo ya elimu ya juu.

"Kweli nimepata tafsiri kuwa mikopo ya elimu ya juu haina upendeleo na jambo la msingi ni mwombaji kujaza fomu kwa usahihi na kuwasilisha maombi yake kwa wakati," alisema Yoctan.

Aidha, Yoctan aliwasihi wanafunzi wahitaji kujitokeza katika mafunzo yanayoendeshwa na HESLB ili kujiongezea uelewa wa namna ya kujaza fomu za maombi ya mikopo kwani yanasaidia idadi kubwa ya wanafunzi wahitaji.

**"Naishukuru HESLB, kunipanga mkopo kwa 100%. Mafunzo ya mwaka 2020 yalinisaidia sana, kwa hali ya kiuchumi ya familia yangu ingekuwa ngumu kumudu gharama za elimu..."**

**alisema Yoctan**

# 2020/2021 WANAFUNZI: NI BAJETI YENU

Na Eline Maronga
Dodoma

"NI bajeti ya kazi na kazi Iendelee", ni maneno ya Maafisa Madawati ya Mikopo katika taasisi za Elimu ya Juu nchini wakipongeza hatua ya Serikali kutenga kiasi cha TZS 570 Bilioni kwa ajili ya bajeti ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kwa mwaka wa masomo 2021/2022.

Kufuatia juhudi hizo, Maafisa Madawati ya Mikopo katika Taasisi za Elimu ya Juu nchini wametoa maoni mbalimbali ya kuipongeza Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia mara baada ya kuwasilishwa kwa hotuba ya makadirio ya bajeti kwa mwaka 2021/2022.

**Kwa mfano, hapa DUCE asilimia 87% ya wanafunzi walikuwa wanufaika kwa mwaka wa masomo 2020/2021, kwa ongezeko hili la bajeti kwa mwaka 2021/2022 tunatarajia kuwa asilimia 95% ya wanafunzi watakuwa wanufaika. Hii inatia matumaini kuwa serikali ina dhamira ya dhati ya kuhakikisha kila mtanzania anapata Elimu bora" anasema Salmon.**

Afisa Mikopo wa Chuo Kikuu Kishirikishi cha Elimu Dar es Salaam (DUCE) Daudi Salmon alisema ongezeko hilo la bajeti litasaidia kupunguza malalamiko ya baadhi ya wanafunzi kukosa mikopo na kuwapunguzia wazazi msongo wa mawazo katika kusomesha vijana wao.

"Kwa mfano, hapa DUCE asilimia 87% ya wanafunzi walikuwa wanufaika kwa mwaka wa masomo 2020/2021. Kwa ongezeko hili la bajeti tunatarajia kuwa asilimia 95% ya wanafunzi watakuwa wanufaika. Hii inatia matumaini kuwa serikali ina dhamira ya dhati ya kuhakikisha kila mtanzania anapata elimu bora" anasema Salmon.

Kwa upande wa Afisa Mikopo wa Chuo Kikuu Kishirikishi (JUCO) Mkoani Morogoro, Sarah Ayoub alisema ongezeko hilo la bajeti litaongeza hali ya utulivu vyuoni na kumwezesha Afisa Mikopo kufanya kazi kwa umakini mkubwa. "Mikakati yetu kama Chuo ni kuhakikisha tunafuata maagizo yanayotolewa na HESLB na kuyatekeleza kwa maslahi ya wanafunzi wetu" alisema Sarah.

Naye Kennedy Mhema, Afisa Mikopo wa Chuo Kikuu Kishirikishi cha Elimu Mkwawa (MUCE) Mkoani Iringa, alisema ongezeko la bajeti litasaidia kuongea idadi ya wanufaika na kuwawezesha wanafunzi wenye uhitaji kutoka kaya maskini kutimiza ndoto zao za kujiunga na masomo ya elimu ya juu.

Akiwasilisha Hotuba ya Makadirio ya Bajeti ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2021/2022, Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako alisema Serikali imetengeza kiasi cha TZS 570 Bilioni ajili ya bajeti ya mikopo ya elimu ya juu katika mwaka wa masomo 2021/2022.

Alisema bajeti hiyo ya masomo inatarajia kusomesha jumla ya wanafunzi wahitaji 160,000 na kuongeza kuwa Serikali itahakikisha wanafunzi wahitaji wanaokidhi sifa na vigezo watapangiwa mikopo yao.





# KITIKU; UDOSO TUTAENDELEA KUUNGA MKONO SERIKALI

Na Ismail Ngayonga
Dodoma

RAIS wa Jumuiya ya Serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu Dodoma (UDOSO), Daudi Kitiku amesema Jumuiya hiyo itaendelea kuiunga mkono Serikali kupitia HESLB kutokana na kulipa fedha na stahiki zote malipo ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kwa wakati.

Akizungumza katika mahojiano maalum na HESLB Yako, Kitiku alisema katika kipindi cha miaka sita (2015-2021) fedha za mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu zimekuwa zikifika kwa wakati na hivyo kuimarisha hali ya utulivu na umakini kwa wanafunzi.

"Serikali, imekuwa ikiongeza bajeti ya mikopo mwaka hadi mwaka, mfano bajeti ya mwaka 2014/2015 ilikuwa TZS 348 Bilioni na ikaongezeka hadi TZS 464 Bilioni mwaka 2020/2021 na katika bajeti ijayo ya mwaka 2021/2022 itakuwa TZS 570 Bilioni, ongezeko hili limepanua wigo kwa vijana wa Kitanzania kupata fursa ya kujiunga na masomo ya elimu ya juu", alisema Kitiku.

Aidha Kitiku alipongeza mfumo wa malipo ya mikopo kwa njia ya alama za vidole (DIDIS) ambao umewezesha fedha za mikopo kuweza kuwafika moja kwa moja kwa wanafunzi wahitaji na hivyo kuongeza imani ya wanafunzi kwa HESLB.

Kitiku alisema UDOSO pamoja na Jumuiya nyingine za wanafunzi wa elimu ya juu nchini, Imekuwa Ikipata ushirikiano mkubwa kutoka HESLB kupitia ushirikiano na Maafisa Madawati ya Mikopo Vyuoni ambao kwa muda wote wamekuwa wakishughulikia changamoto mbalimbali za wanafunzi.

"Pamoja na juhudi hizo za HESLB, Jumuiya na Serikali za wanafunzi pia zimekuwa zikipata ushirikiano mkubwa kutoka kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo ndiyo mlezi wetu katika kusimamia ustawi wa sekta ya elimu ya juu nchini" alisema Kitiku.



## MHE. HEMEDI
# TAHLISO; KAZI NZURI

**Na Mwandishi Wetu**
**Zanzibar**

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, ameupongeza uongozi wa TAHLISO kwa ushirikiano mkubwa ulioisaidia serikali kuweza kutatua changamoto zinazowakabili wanafunzi wa taasisi za elimu ya juu nchini ikiwemo mikopo ya elimu ya juu.

Mhe. Hemed aliyasema Mei 25 mwaka huu wakati akizungumza na viongozi wa taasisi hiyo waliomaliza muda wao na kuwatambulisha viongozi wapya waliochaguliwa wakati walipofika ofisini kwake Vuga Zanzibar.

Alisema TAHLISO imeendelea kufanya kazi nzuri na kupata mafanikio makubwa katika kuratibu masuala mbalimbali ya wanafunzi wa vyuo vikuu nchini na hivyo kusaidia maendeleo ya vyuo vikuu nchini.

Aidha, Mhe. Hemed aliwataka viongozi hao kuendeleza mahusiano na ushirikiano kati yao na serikali ili Taifa liweze kupata maendeleo hasa katika sekta ya elimu, na kuwaeleza kuwa Serikali inawaamini vijana kwa mchango wao mkubwa wanaoutoa kwa taifa.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar aliwaasa viongozi wapya wa taasisi hiyo waliochaguliwa kujenga uzalendo na kudumisha falsafa ya uwajibikaji kwa kuunga mkono jitihada za viongozi wa serikali.

Mapema Mwenyekiti mstaafu wa TAHLISO, Peter Niboye alimpongeza Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa jitihada zake anazozichukua katika kukuza sekta ya elimu nchini, na kueleza katika uongozi wao wamefanikiwa kutatua changamoto mbali mbali za wanafunzi.

**Alisema TAHLISO imeendelea kufanya kazi nzuri na kupata mafanikio makubwa katika kuratibu masuala mbalimbali ya wanafunzi wa vyuo vikuu hususani suala la mikopo ya wanafunzi na hivyo kusaidia ukuaji na maendeleo ya vyuo vikuu nchini.**



# MCHANGO WA HESLB ELIMU YA JUU UGHAIBUNI

**Na Veneranda Malima**
**Dar es salaam**

Imebainishwa kuwa wanafunzi wa Kitanzania wanaosoma nje ya nchi licha YA kupata elimu kwa lengo la kuziba pengo la uhaba wa wataalam katika baadhi ya kada nchini lakini pia wametanua wigo wa uelewa wao katika masuala ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kidiplomasia.

Akizungumza na HESLB Yako, Mkurugenzi wa Uchambuzi na Utoaji Mikopo Dkt Veronica Nyahende amesema kuwa kusoma nje ya nchi ni fursa ya wanafunzi wa Kitanzania kupata elimu na wakati huohuo wakijifunza masuala mengine ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kidiplomasia kwa faida ya nchi.

"Suala la kwanza kwa umuhimu ni kupata elimu ili kuziba pengo la uhaba wa ujuzi (skills gap), mengine ni kujifunza masuala ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kuboresha ushirikiano wa kidiplomasia hasa na nchi marafiki ambako wanafunzi hao wanakwenda kupata elimu", amesema Dkt Nyahende.

Serikali imekuwa na utaratibu kupitia HESLB, kulipia sehemu ya gharama za masomo ya wanafunzi wa Kitanzania wanaokwenda kusoma nje ya nchi ikiwa ni pamoja na tiketi za kwenda na kurudi pamoja na fedha za kujikimu. Utaratibu huo ulianza mwaka 2010/2011 kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kutangaza nafasi za skolashipu kutoka kwa nchi marafiki wa Tanzania.

Kufikia mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali imeshatumia kiasi cha TZS 62.8 bilioni kuwanufaisha mamia ya wanafunzi wa Kitanzania ambao wengi wao tayari wanaitumikia nchi kama wataalam katika nafasi mbalimbali.


Mmoja wa wanufaika wa skolashipu za Serikali, Viatory Kazana Mnyaga (34) aliyehitimu Shahada ya Utawala katika Elimu kutoka Chuo Kikuu cha Pedagogica nchini Msumbiji mwaka 2019, amekiri kuwa licha ya elimu aliyoipata, amenufaika na mambo mengi. Baadhi yake ameyataja kuwa ni pamoja na kujifunza lugha mpya ya kigeni (Kireno), kukutana na kushirikiana na watu wa mataifa mbalimbali na kuongeza haiba yake katika kujiamini.

Wanafunzi wa kitanzania wamekuwa wakienda nje ya nchi kusoma shahada katika fani mbalimbali zikiwemo udaktari wa tiba ya binadamu, udaktari wa tiba ya mifugo, utaalam wa kilimo biashara, usanifu wa majengo na mifumo ya utalii na hoteli.

HESLB imekuwa ikitoa sehemu ya fedha kama mikopo ama ruzuku kwa niaba ya serikali kwa nyakati tofauti kwa wanafunzi wanaosoma katika baadhi ya nchi wahisani na marafiki wa Tanzania zikiwemo China, Russia, Algeria, Msumbiji, Cuba, Misri, Ujerumani, Uturuki na Ukraine. Nchi nyingine ni Uganda, Serbia, Poland, Malaysia, Czech, Afrika Kusini na India.

Nchi ambazo kwa sasa zina Wanafunzi wanaoendelea na masomo na idadi yao kwenye mabano ni Algeria (40), Cuba (1), Msumbiji (40) na Russia (23).

**"Suala la kwanza kwa umuhimu ni kupata elimu ili kuziba pengo la uhaba wa ujuzi (skills gap), mengine ni kujifunza masuala ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kuboresha ushirikiano wa kidiplomasia hasa na nchi marafiki ambako wanafunzi hao wanakwenda kupata elimu", amesema Dkt Nyahende.**






# WAMBURA: TUPO 'STANDBY' TUPO KAMILI

**Na Jacqueline Msuya**
**Dar es salaam**

Kitengo cha TEHAMA HESLB kimesema kimekamilisha maandalizi ya kufunguliwa kwa dirisha la maombi ya mikopo ya elimu ya juu kwa mwaka 2021/2022 kwa njia ya mtandao (OLAMS) linalotarajiwa kufunguliwa mapema mwezi Julai 9 mwaka huu.

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa TEAHAMA, Didas Wambura anaiambia HESLB Yako kuwa, kitengo hicho tayari kimepokea mahitaji yote ya msingi yanayohitajika kutoka Idara ya Uchambuzi na Upangaji Mikopo DLAD kwa ajili ya kuingiza taarifa kwenye mifumo ya TEHAMA.

"Kila mwaka huwa tunakutana na Ofisi ya DLAD kwa ajili ya kuangalia marekebisho ya msingi kabla ya kufunguliwa kwa dirisha la maombi kwa njia ya mtandao kupitia OLAMS, ambalo ndio dirisha la wanafunzi kwa ajili ya kupokea maombi ya mikopo" alisema Wambura.

Kwa mujibu wa Wambura, timu ya wataalamu ya TEHAMA tayari imefanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa na Ofisi ya DLAD kuwataka wanafunzi wahitaji kuwa tayari na kuandaa mahitaji ya msingi ya maombi ya mkopo kwa mujibu wa mwongozo.

Aidha Wambura alisema kwa mwaka 2021/2022 Kitengo hicho kimepanga mikakati mbalimbali katika kuhakikisha kuwa unaongeza ufanisi na utendaji wa mfumo wa OLAMS kuwa imara na kuwawezesha wanafunzi wahitaji kutuma maombi yao kwa haraka na wepesi zaidi.

Aliongeza kuwa Kitengo cha TEHAMA pia kipo katika maandalizi ya uboreshaji wa mifumo mbalimbali ya kitaasisi ili kuwa na mfumo wezeshi utakaosaidia utoaji huduma mbalimbali kwa wateja kupitia njia mbalimbali za mtandao ikiwemo simu ya mkononi.

"Tumejipanga katika kuhakikisha kuwa kufikia mwaka 2022 tunakuwa na dirisha la huduma za mtandao, ambazo zitasaidia wateja wetu kupata huduma kupitia simu za mkononi ambazo zitaongeza ufanisi na utendaji kazi wa taasisi yetu", alisema Wambura.

Akifafanua zaidi Wambura alisema HESLB pia imejipanga kuimarisha ushauriano na wadau wa kimkakati ikiwemo TASAF, NIDA, RITA na ZHELB ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa na vielelezo mbalimbali vya wanafunzi wahitaji vinavyohitajika wakati wa dirisha la maombi na urejeshaji wa mikopo.

**"Tumejipanga kufikia mwaka 2022 tutakuwa na dirisha la huduma zetu kwa njia ya mtandao (HESLB Getway), ambalo litahusisha uombaji na urejeshaji wa mikopo na mifumo ya malipo ya ndani kupitia simu za mkononi ambapo tutaongeza ufanisi na utendaji kazi wa taasisi yetu"**

**alisema Wambura**



# TUTAWATAFUTA, TUTAWAFIKIA, TUTAWADAI, KISTAARABU

**Na Mwandishi Wetu**
**Mwanza**

HESLB imesema imejiwekea mikakati madhubuti ya kuongeza makusanyo na kuendelea kutumia mbinu mbadala za kubaini wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu nchini

Mkurugenzi wa Urejeshaji na Urejeshwaji Mikopo (HESLB) George Mziray alisema kufuatia maelekezo yaliyotolewa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jahmuri ya Muungano wa Tanzania ya kuendelea na makato ya 15% ya kiwango cha mshahara wa wanufaika, tayari HESLB imeweka mikakati ya kufikia malengo ya makusanyo na kubaini wanufaika.

"Tumejiwekea mikakati madhubuti ya kuongeza makusanyo na kubaini wanufaika wengi Zaidi, kufuatia maelekezo yaliyotolewa na Mhe. Rais, Samia Suluhu Hassan na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof. Joyce Ndalichako ya kufutwa kwa adhabu na tozo za mkopo", alisema Mziray.

Alisema kuwa kupitia Kamati maalum iliyoundwa na HESLB kupitia hoja, ushauri na mapendekezo hayo tayari yameanza kufanyiwa kazi ili kuhakikisha kuwa wanufaika wanarejesha mikopo .

Kwa mujibu wa Mziray alisema katika mwaka 2021/2022 HESLB imejipanga kuhakikisha inaimarisha mahusiano na wadau wa kimkakati ikiwemo Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Ofisi ya Rais Tawala za Miko na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na wadau wengineo ili kuweza kurahisisha upatikanaji wa taarifa mbalimbali za wanufaika.

Akizungumza katika maadhimisho ya siku ya Wafanyakazi Duniani,Jijini Mwanza, Rais Samia Suluhu Hassan alitoa maelekezo kwa HESLB kufuta tozo ya 6% ya kulinda thamani ya mkopo (VRF) na kuwataka wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu kuendelea kurejesha mikopo hiyo kwa makato ya 15% ya mashahara kwa wanufaika waliopo katika ajira rasmi.

Aidha, Mhe. Rais aliipongeza HESLB kwa kuongeza kasi ya makusanyo ya mikopo kwa wanafunzi kutoka TZS 28 Bilioni mwaka 2015/16 hadi kufikia TZS 192 Bilioni mwaka 2019/2020 na kuwataka wanufaika waliopo katika ajira rasmi kuendelea kurejesha mikopo hiyo kwa kiwango cha makato ya asilimia 15 kutoka katika mishahara yao.

**"Tumejiwekea mikakati madhubuti ya kuongeza makusanyo na kubaini wanufaika wengi Zaidi, kufuatia maelekezo yaliyotolewa na Mhe. Rais, Samia Suluhu Hassan na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof. Joyce Ndalichako ya kufutwa kwa adhabu na tozo za mkopo", alisema Mziray.**

# UONGOZI MPYA TAHLISO WAIPONGEZA SERIKALI

**Na Jacqueline Msuya**
**Dar es Salaam**

Jumuiya ya Wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu Nchini (TAHLISO), imepongeza juhudi zinazofanywa na Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) katika kuongeza bajeti na idadi ya wanufaika wa mikopo ya juu nchini.

Akizungumza katika mahojiano maalum na HESLB Yako, Mwenyekiti mpya wa TAHLISO, Frank Nkinda anasema katika kipindi cha miaka sita HESLB imeendelea kutumia mifumo imara ya kitaasisi inayowezesha wanafunzi wenye sifa na vigezo kupangiwa mikopo.

Nkinda aliongeza kuwa TAHLISO inatambua hoja na changamoto za wanafunzi, hivyo itaendelea kushirikiana na HESLB pamoja na viongozi wa Serikali za wanafunzi ili kuzipatia ufumbuzi wa kudumu.

Akifafanua zaidi Nkinda alisema TAHLISO inatambua taasisi mafanikio makubwa yaliyotekelezwa na HESLB katika kuwawezesha wanafunzi wahitaji kutoka familia maskini, hivyo uongozi mpya wa TAHLISO utahakikisha unaendelea kuenzi mafanikio hayo.

AlisemaTAHLISO inatambua wajibu mkubwa ilionao katika kuratibu, kupokea na kushughulikia hoja zote za wanafunzi hususani suala la mikopo ya elimu ya juu, hivyo TAHLISO itahakikisha maoni hayo yanafikishwa katika ngazi husika na kupatiwa ufumbuzi.

"TAHLISO tuna wajibu wa kuishauri Serikali na kuwasilisha hoja, maoni ya wanafunzi pale yanapojitokeza na tunapaswa kutumia hekima na busara katika kuziwasilisha, hili ni jukumu linalopaswa kufanywa na viongozi wote wa jumuiya ya serikali za wanafunzi" alisema Nkinda.

Nkinda alisema TAHLISO itaendelea kushirikiana na taasisi zote za serikali zinazohusika na sekta ya elimu ya juu nchini ikiwemo Tume ya Vyuo Vikuu (TCU), HESLB na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE).



# NIBOYE; UONGOZI KUPOKEZANA



**Na Jacquiline Msuya**
**Dodoma**

MWENYEKITI Mstaafu wa Jumuiya ya Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu (TAHLISO), Peter Niboye, amempongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kwa utendaji kazi wake uliotukuka na kusisitiza kuwa vyuo hivyo vitaendelea kuwa maeneo salama.

Akizungumza katika mahojiano maalum na HESLB YAKO, Niboye anasema Serikali imefanya jitihada mbalimbali za kuhakikisha Watanzania wa hali ya chini wanapata Elimu ikiwemo kuongeza bajeti ya elimu ya Juu kufikia TZS 500 Bilioni kwa mwaka wa masomo 2021/2022.

Niboye anasema kwa muda mrefu sasa suala la migomo na maandamano ya wanafunzi wa elimu ya juu limedhibitiwa kutokana na kuwepo kwa uongozi imara wa wanafunzi wenye uwezo wa kushughulikia changamoto zao ikiwemo kupata fedha za mikopo kwa wakati.

Akizungumzia siri ya utulivu kwenye vyuo hivyo, Niboye anasema uongozi wake umeshughulikia changamoto mbalimbali zilizokuwa zikiwakabili wanafunzi na kurudisha imani ya jumuiya hiyo na taasisi mbalimbali za serikali.

"Nimeongoza taasisi hii bila maandamano tangu mwaka 2018 nilipoingia madarakani hii ni kwa sababu mimi pamoja na viongozi wenzangu tuliamua kutambua majukumu yetu ya kutatua changamoto za wanafunzi na kufanya ziara za mara kwa mara vyuoni" anasema Niboye.

Kwa mujibu wa Niboye anasema hadi anapomaliza muda wa uongozi wake tayari ametembelea jumla ya vyuo vikuu na vya kati 201, ambapo wakati wa uongozi wake alihakikisha anatumia muda na nguvu yake kubwa katika kuhakikisha viongozi wote wanajitambua na kuisadia serikali.

Akifafanua zaidi, Niboye anasema wakati wa uongozi wao walijitahidi sana kurejesha imani ya TAHLISO kwa taasisi za Serikali ambazo wanafanya nazo kazi ikiwemo TCU, HESLB, NACTE, NHIF na taasisi nyingine ikiwemo Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

# JUSTA; HESLB MLEZI WA WANA



**Na Mwandishi wetu**
**Dar es salaam**

FARAJA katika maisha ni mwanzo mpya wa nuru na mwanga wa safari ya mafanikio ya mwanadamu.

Zipo methali za kiswahili ambazo zinaakisi nadharia ya faraja, Justa Joseph (21) anathibitisha kuwa ni kweli "Baada ya dhiki faraja" kufuatia msiba wa wazazi wake Joseph Kazoba na Laurensia Pastory.

Simulizi ya Justa Joseph (21), Mwanafunzi wa mwaka wa kwanza wa Chuo Kikuu Ardhi (ARU), inafafanua dhana ya HESLB katika utoaji na upangaji wa mikopo kwa wanafunzi wahitaji, kama anavyojieleza katika mahojiano maalum kati yake na HESLB Yako.

"Ni mtoto wa pekee katika familia yetu ya watoto saba ambao ni yatima, niliyebahatika kufika masomo ya chuo kikuu, wenzangu walikata tamaa na kuishia njiani. Binafsi nilijipa moyo na kumtanguliza Mungu, naishukuru HESLB kwa kuja kuwa mkombozi wa familia yetu", alisema Justa.

Akifafanua zaidi Justa anasema alipopata taarifa ya kuchaguliwa kujiunga na ARU alijawa na wasiwasi kutokana na uyatima na hali ya kiuchumi ya familia yakeilikuwa duni kidogo, na hivyo anaishukuru Serikali kupitia HESLB haikumuacha mkiwa ilimpangia mkopo wa elimu ya juu kwa asilimia 100.

Justa alisema mwaka 2020, wakati HESLB ilipotoa mwongozo na kufungua dirisha la maombi ya mkopo wa elimu ya juu mwaka 2020, alijitahidi kujaza fomu kwa usahihi, kutuma kwa wakati na kuambatisha nyaraka mbalimbali zilizohitaji.

Anazitaja moja ya nyaraka hizo kuwa ni pamoja na cheti cha kuzaliwa na vyeti vya vifo vya wazazi wake, vilivyohakikiwa na RITA pamoja na kuhakiki usahihi wa maombi yake kabla ya kutuma kwa njia ya mtandao.

"Binafsi nilipohitimu masomo ya kidato cha sita, Shule ya Sekondari Josiah Girls ambayo ni shule binafsi iliyopo Wilaya ya Bukoba mwaka 2020, nilipata daraja la I, niliamini kuwa nitapangiwa mkopo kutokana na sifa za uhitaji zilizoanishwa katika mwongozo zilienda sambamba na uhalisia wangu" alisema Justa.

Ailihitimisha kwa kuipongeza HESLB kwa kuwa na mfumo wenye uwazi katika utoaji na upangaji wa mikopo na kuwataka wanafunzi wahitaji kuondokana na dhana ya kuwa wanafunzi waliosoma shule binafsi hawapangiwi mikopo ya elimu ya juu.


## OFISI ZETU

### DAR ES SALAAM
BODI YA MIKOPO YA WANAFUNZI ELIMU YA JUU
HESLB HOUSE, 1 MTAA WA KILIMO, TAZARA, BR. MANDELA.
S.L.P 76068, 15471 DAR ES SALAAM
0736 665533 | 0739 665533
INFO@HESLB.GO.TZ

### DODOMA
JENGO LA CAG, GHOROFA YA CHINI,
S.L.P 984, DODOMA,
SIMU: 0758 067 577 | 0739 067 577
DODOMA@HESLB.GO.TZ

### ZANZIBAR
JENGO LA ZSTC, KINAZINI, BR. MALAWI,
S.L.P 900, ZANZIBAR,
SIMU: 0779 321 424
ZANZIBAR@HESLB.GO.TZ

### ARUSHA
NSSF JENGO LA MAFAO, GROROFA YA KWANZA,
S.L.P 2712, ARUSHA,
SIMU: 027 2520128 | 0624 100011 | 0739 102016
ARUSHA@HESLB.GO.TZ

### MWANZA
PSSSF PLAZA, GROROFA YA PILI,
FRONT WING, BR. KENYATTA, S.L.P 3051, MWANZA,
SIMU: 028 2506008 | 0759 819350 | 0738 153661
MWANZA@HESLB.GO.TZ

### MBEYA
JENGO LA CAG, BR. MBALIZI,
S.L.P 319, MBEYA,
SIMU: 0738 131310 | 0738 131311
MBEYA@HESLB.GO.TZ

### MTWARA
NHC RAHA LEO COMPLEX GROROFA YA PILI
KIWANJA NA. 217 KITALU H,
KARIBU NA OFISI YA MKUU WA MKOA
S.L.P 969, MTWARA, SIMU: 0736 026 668
MTWARA@HESLB.GO.TZ